**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**TUME YA UTUMISHI SERIKALINI**

**Kumb.Na.BA.1/25/01A/12** **20 Januari, 2026**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Tume ya Utumishi Serikalini inatangaza nafasi za kazi kwa ajili ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kama ifuatavyo:-

**1. Afisa Tathmini ya Uchumi wa Mafuta na Gesi Daraja la II (ZPSG-08) Nafasi 1 – Unguja**

Sifa za Muombaji:

- Awe Mzanzibari mwenye umri usiozidi miaka arobaini na sita (46).
- Awe na vyeti halisi vya kumaliza masomo.
- Awe amehitimu elimu ya shahada ya kwanza ya Uchumi wa Mafuta na Gesi (Petroleum Economist) au Shahada ya kwanza ya Jiolojia ya Mafuta na Gesi (Petroleum Geology) au Shahada ya kwanza ya Mhandisi wa Mafuta na Gesi Asilia (Petroleum Engineer) kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na uwezo mzuri wa kutumia kompyuta.

**2. Afisa Uvuvi Msaidizi Daraja la III (ZPSD-03) Nafasi 8 – Pemba**

Sifa za Muombaji:

- Awe Mzanzibari mwenye umri usiozidi miaka arobaini na sita (46).
- Awe na vyeti halisi vya kumaliza masomo.

- Awe amehitimu Stashahada ya Uvuvi au Stashahada ya Sayansi ya Uvuvi au Stashahada ya Kilimo cha Bahari au Stashahada ya Sayansi ya Bahari au Stashahada ya Teknolojia ya Uvuvi kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na uwezo mzuri wa kutumia kompyuta.

**3. Mhandisi Majengo Daraja la II (ZPSG-08) Nafasi 1 – Unguja**

Sifa za Muombaji:

- Awe Mzanzibari mwenye umri usiozidi miaka arobaini na sita (46).
- Awe amehitimu Shahada ya Kwanza ya Uhandisi Majengo kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na uwezo mzuri wa kutumia kompyuta.

**4. Afisa Uvuvi Msaidizi Daraja la III (ZPSD-03) Nafasi 10 – Unguja**

Sifa za Muombaji:

- Awe Mzanzibari mwenye umri usiozidi miaka arobaini na sita (46).
- Awe amehitimu Stashahada ya Uvuvi au Stashahada ya Sayansi ya Uvuvi au Stashahada ya Kilimo cha Bahari au Stashahada ya Sayansi ya Bahari au Stashahada ya Teknolojia ya Uvuvi kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na uwezo mzuri wa kutumia kompyuta.

## ***Jinsi ya Kuomba:***

Maombi yote yawasilishwe kwa njia ya Kielektroniki kwenye mfumo wa Maombi ya Ajira (ZanAjira) kupitia anuani ifuatayo:

**https://portal.zanajira.go.tz** kuanzia tarehe **20 Januari, 2026** hadi tarehe **03 Febuari, 2026**.

- Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Tume ya Utumishi Serikalini **www.zanajira.go.tz**.
- Barua za maombi zitumwe kwa anuani ifuatayo kupitia mfumo wa ZanAjira (kwa njia ya kielektroniki pekee):-

  **KATIBU,**
  **TUME YA UTUMISHI SERIKALINI,**
  **S.L.P 1587,**
  **ZANZIBAR**
- Muombaji anatakiwa kuainisha nafasi ya kazi anayoiomba.
- Muombaji atakaewasilisha “Progressive Report” au “Statement of Results” pekee maombi yake hayatazingatiwa.
- Kwa msaada wa kitaalamu wasiliana na Tume ya Utumishi Serikalini kupitia simu Nam. 0773101012.

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:**
**KATIBU,**
**TUME YA UTUMISHI SERIKALINI.**
**ZANZIBAR**